NDOA TAKATIFU

MAFUNDISHO

Ndoa, yaani mapatano kati ya mume na muke kuishi pamoja, inajulikana katika mataifa karibu yote duniani. Lakini desturi ni mbalimbali.

Ndoa takatifu ni ndoa kufuatana na mapenzi ya Mungu, na inaweza kuwa tofauti na ndoa ya kawaida:

Katika ndoa takatifu mume na muke wanajitoa kabisa, mumoja kwa mwingine, sawa vile Yesu alijitoa musalabani, na kanisa linajitoa kumufuata. Kila mumoja anajitoa kutimiza mahitaji ya mwenzake, kujua na kufahamu mwenzake, na kumufurahisha.

Ndoa takatifu ni ndoa yenye kusimama imara, kwani mume na muke wanaahidi kubaki pamoja katika mapendo mpaka kufa; ukubwa wa ahadi hii unaleta uhodari kwao, na kwa watoto wao, na kwa wengine, katika dunia yenye mageuko mengi.

Kufunga ndoa takatifu, mutu anaacha baba yake na mama yake. Ni kusema, sasa kazi ya kwanza ya mume na muke ni kutunzana na kutunza watoto wao. Wangali wanapaswa kuheshimu wazazi wao, lakini wazazi hawana uwezo juu yao sawa mbele.

Ndoa takatifu ni mapatano kati ya mume mumoja, muke mumoja, mbele ya Mungu Mwenyezi. Mapaswa ya ndoa takatifu ni kali, lakini wakristo wanapata nguvu toka Muumba wa dunia na mbingu.

Mume ni kichwa cha muke, akamupenda muke wake sawa anavyopenda mwili wake mwenyewe, na muke anatii mume sawa kanisa linatii Kristo.

MAAGIZO

A Wakati mwanamume na mwanamuke wanaomba kufunga ndoa yao kanisani, Muchungaji wa parokia ajifunze juu ya matayarisho yao, na mafikiri ya jamaa zao. Apime kufahamu vitu gani vinaweza kuzuiza ndoa ya furaha na kudumu. Awaombee, kwao na kwake.

B Ndoa takatifu ni kwa wakristo. Lazima wachumba wawili wote wabatizwe mbele ya kuandikisha ndoa.

C Kasisi anapaswa kufundisha wachumba maana ya ibada hii, na desturi ya wakristo walioungana ndani ya ndoa takatifu; lakini anaweza kuita wakristo wengine kumusaidia kwa kazi hii. Mafundisho yafuate programme iliyokubaliwa na Dayosisi.

D Inafaa kutangaza ndoa kanisani kwa yenga tatu wakati wa ibada ya kawaida. Muhudumu aseme hivi:

> Ninatangaza habari za ndoa ya *Fulani* wa parokia *Fulani,* mutoto wa *Fulani* na *Fulani* wa kijiji/muji *Fulani,* na *Fulani* wa parokia *Fulani,* mutoto wa *Fulani* na *Fulani* wa kijiji/muji *Fulani*. Hii ni mara ya kwanza (*au* pili, *au* tatu) ya kuuliza. (Vilevile habari ya ndoa ya Fulani...)
> Mutu wo wote kati yenu akijua sababu au zuizo la haki ili watu hawa wasiunganishwe katika ndoa takatifu, lazima aseme.

Ikiwa mutu analeta zuizo, au mbele ya siku ya kufunga ndoa au kati yake, Muchungaji wa parokia ajifunze haki juu yake, akiomba uongozi wa Mungu. Ikiwa haoni wazi namna kuendelea, anaweza kuleta lile neno mbele ya kamati (duwani) ya parokia, ikate shauri. Ikiwa mutu analeta neno kwa siku ya ndoa yenyewe, Muchungaji ashirikiane na Serikali kwa uchunguzi wa zuizo lile.

E Ndoa ifanyike kwa saa za muchana, na washuhuda wawe wawili au wengi zaidi. Ni vema kama baba za wachumba wanawatoa kwa kuoana; lakini mwingine katika jamaa yake, au mujumbe wa jamaa, anaweza kusimama pahali pa baba.

F Mwenye mamlaka kufunga ndoa takatifu ni Muchungaji wa parokia, au Askofu wa Dayosisi. Lakini Muchungaji anaweza kuruhusu kasisi au dikoni mwingine kuifanya, au kuhubiri, au kuongoza maombi.

G Wachumba wanaweza kusoma viapo vyao, au kuvisema nyuma ya muhudumu, mustari kwa mustari; na vilevile maneno ya pete..

H Mume na muke wanapeana pete sawa alama za ndoa yao. Pengine alama nyingine zinaweza kutumiwa pahali pa pete, kufuatana na desturi za zamani

za jamaa ya mume au muke. Ikiwa pete (au alama) ni moja tu, mume aipatie muke.

I Mwenye kuhubiri achague vipande vya Maandiko Matakatifu vitakavyosomwa; anaweza kuvichagua pamoja na wachumba. Vipande vinavyofaa ni hivi, lakini vingine vinawezekana:

AGANO LA KALE:

Mwanzo 1:26-28	Mwanzo 2:18-25
Mwanzo 24:42-58	Yosua 24:42-58
Mezali 31:10-17, 26-31	Muhubiri 4:9-12

AGANO JIPYA:

Matendo 18:24-26	Roma 12:1-2, 9-18
1 Wakorinto 13:1-13	Waefeso 4:25 - 5:2
Waefeso 5:21-33	Wakolosayi 3:12-17
1 Petro 3:1-9	1 Yoane 4:7-16

HABARI NJEMA:

Matayo 5:25-34	Matayo 19:3-6
Luka 6:46-49	Yoane 2:1-11
Yoane 15:1-13	

J Ikiwa wazazi wataleta mashauri kwa N° 25, inafaa wayaeleze kwa kasisi mbele ya ibada.

NDOA TAKATIFU

1* *Wachumba na wasaidizi wao wanaweza kuingia kanisa na wimbo wa furaha.*

2 *Wahudumu waingie, na kasisi akaribishe wageni na maneno machache.*

3 *Shairi moja la Biblia lisomwe, au hili:*

Mungu ni mapendo, naye anayekaa katika mapendo, anakaa ndani ya Mungu, na Mungu anakaa ndani yake. *1 Yoane 4:16*
Au hili:

Itasikilika tena sauti ya furaha, na sauti ya kicheko, na sauti ya bwana arusi, na sauti ya bibi arusi, sauti yao wanaosema: Musifu Bwana wa majeshi, maana Bwana ni mwema, rehema zake ni za milele. *Yeremia 33:11*

4 *Kasisi aseme:* Tuombe.

Mungu Baba yetu,
umetufundisha ya kwamba
mapendo ni utimilifu wa sheria.
Uwape watumishi wako hawa wenye kupendana,
waendelee kudumu katika mapendo yako,
hata mwisho wa maisha yao:
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

5 *Vipande viwili au vitatu vya Maandiko Matakatifu visomwe. Musomaji atangaze kila kipande sawa kwa wakati wa Ushirika Mutakatifu. Ikiwa Ushirika Mutakatifu utakuwa, lazima kipande cha mwisho kiwe Injili.*

6 *Kuhubiri*

7* *Wimbo*

8 *Wachumba wasimame mbele ya kasisi. Kasisi aseme:*
Leo tumekusanyika mbele ya Mungu, kushuhudia Ndoa ya J. na J., kuomba baraka ya Mungu juu yao, na kufurahi pamoja nao.

Mungu aliunda hali ya ndoa tangu zamani. Mume mumoja na muke mumoja wanaacha wazazi wao, na wanaanza maisha mapya, wakitoleana maisha yao, wakiungana katika mwili na katika roho.

Ndoa imetolewa ili mume na muke wafarijiane na wasaidiane katika uaminifu siku zote, pasipo mutu mwingine kuwatenga.

Ndoa imetolewa ili mume na muke wajuane katika furaha ya maungano ya miili yao, pasipo kunyimana, na hivi kupata nguvu na umoja kwa utumishi wao.

Ndoa imetolewa ili mume na muke wapate baraka ya kuzaa na kutunza watoto katika starehe, na kuwakomelesha katika imani.

Tunajua kwamba pasipo Mungu sisi watu hatuna salama, hatuna uwezo. Vilevile mume na muke hawawezi kutimiza mapaswa ya ndoa pasipo kutii na kutegemea Bwana.

Hawa wawili wamechagua kuishi pamoja katika ndoa. Leo tutasikia namna wanakubaliana; watashikana mikono na kuapiana viapo; alama za ahadi zao zitapewa; na sisi sote tutaomba Mungu kuungana nao, kuwaongoza na kuwawezesha.

9 *Kasisi aulize mwanamume:*
J, unapenda na kutumaini J? Utamutwaa kuwa muke wako, kumutunza na kumutegemeza, katika hali yo yote ya maisha, ukiacha wengine wote?
Mwanamume ajibu:
Ndiyo, nitafanya hivi.
Kasisi aulize mwanamuke:
J, unapenda na kutumaini J? Utamutwaa kuwa mume wako, kumutunza na kumutegemeza, katika hali yo yote ya maisha, ukiacha wengine wote?
Mwanamuke ajibu:
Ndiyo, nitafanya hivi.

10 *Kasisi aulize kanisa:*
Ikiwa mutu wo wote anajua sababu, hawa wawili wasifanye ndoa yao, anapaswa kuisema sasa, au kutoka sasa anyamaze kabisa.
Kasisi aulize mume na muke:
Na kama mumoja wenu anajua sababu, ninyi hamuwezi kuoana kwa halali, inafaa aseme sasa; kwa sababu viapo mutakavyoapa sasa vitaapiwa kwa jina la Mungu, aliye Muhukumu wa wote, na anayejua siri zote za mioyo yetu.
Ikiwa hakuna jibu, kasisi aulize kanisa:
Ninyi ni jamaa, na jirani, na rafiki za J na J.
Mutawategemeza wao katika ndoa yao, mukifanya nguvu kuwasaidia na kuwaombea?
Wote **Ndiyo; tutafanya hivi.**

11 *Kasisi aulize:*
Nani anatoa mume huyu, kuungana na muke huyu, kuanza maisha mapya na kuunda nyumba mpya?
Jibu Mimi ninamutoa; tunamuaga na huzuni, lakini tunafurahi kwa ajili ya ndoa yake.
Mwenye kumutoa anaweza kumukamata kwa mukono na kumuleta karibu na kasisi.

12 *Kasisi aulize:*
Nani anatoa muke huyu, kuungana na mume huyu, kuanza maisha mapya na kuunda nyumba mpya?
Jibu Mimi ninamutoa; tunamuaga na huzuni, lakini tunafurahi kwa ajili yake.
Mwenye kumutoa amukamate kwa mukono na kumuleta karibu na kasisi.

13 *Mume na muke waangaliane. Mume apokee mikono ya muke kwa mikono yake; aseme:*
Mimi J ninakutwaa J
kuwa muke wangu
tangu leo mpaka kufa
kukupenda na kukutunza
na kukuhesimu
katika mema na katika mabaya,
katika utajiri na katika umasikini,
wakati wa ugonjwa na wakati wa uzima;
kwa utakatifu na uaminifu;
na hiki ni kiapo changu.

Waachane mikono; muke apokee mikono ya mume kwa mikono yake; aseme:
Mimi J ninakutwaa J
kuwa mume wangu
tangu leo mpaka kufa
kukupenda na kukutunza
na kukuhesimu
katika mema na katika mabaya,
katika utajiri na katika umasikini,
wakati wa ugonjwa na wakati wa uzima;
kwa utakatifu na uaminifu;
na hiki ni kiapo changu.

Waachane mikono.

14* *Kasisi apokee pete na kuomba baraka ya Mungu:*
Bwana,
uzungushe *pete hizi* na baraka yako,
*zi*funge J na J katika mapendo,
uaminifu na umoja pasipo mwisho.
Wote **Amina.**

15 *Mume na muke wapeane pete, au kama pete ni moja tu mume aipatie muke. Anayeleta pete aseme:*

Na furaha kubwa ninakupa pete hii kuwa alama ya ndoa yetu;
Mungu anisaidie kukupa kila kitu ninacho:
mwili, mali, na mashauri;
katika mapendo ya Baba, Mwana na Roho Mutakatifu.

16 *Kasisi aseme kwa watu wote:*
Mbele ya Mungu na mbele ya mukutano huu,
J na J wamekubaliana na wametoleana viapo vyao vya ndoa. Wametangaza ndoa yao kwa kushikana mikono na kwa kutoa na kupokea pete. Kwa hivyo ninawatangaza kuwa bwana na bibi.

Kasisi ashike mikono yao ya kiume akisema:
Wale Mungu aliowaunganisha, mutu asiwatenganishe.

Watu wote wanaweza kuonyesha furaha yao na nyimbo au vigelegele au namna nyingine yenye kufaa.

17 *Kasisi aseme:* Tuombe!
Mume na muke wapige magoti. Kasisi asimame na aombe baraka hivi:

Mungu Baba,
Mungu Mwana,
Mungu Roho Mutakatifu,
awabariki, awaokoe, awalinde.
Bwana kwa rehema yake awape wingi wa neema yake,
ili mumupendeze
kwa mwili na kwa roho,
na, mukiishi pamoja katika imani na mapendo,
mupate baraka za uzima wa milele.
Amina.

18* *Mashangilio haya yanaweza kutumiwa:*
Kasisi Ubarikiwe, Baba ya mbinguni:
Wote **Unayewapa furaha kwa mume na muke.**
Kasisi Ubarikiwe, Bwana Yesu Kristo:
Wote **Umeletea watu uzima mupya.**
Kasisi Ubarikiwe, Roho Mutakatifu:
Wote **Unatujenga pamoja katika mapendo.**
Kasisi Ubarikiwe, Baba, Mwana na Roho Mutakatifu:
Wote **Mungu mumoja, usifiwe milele. Amina.**

19 *Maombi. Kasisi au muhudumu mwingine aombe, akitumia mbili au zaidi kati ya maombi haya, au maombi mengine.*

A *Kwa umoja katika maisha*

Mungu mwenyezi,
umeumba kila mutu kwa mufano wako na kila mumoja kwa namna yake,
na unaita kila mutu mumoja kumufuata Mwokozi;
tunakusihi kwa neema yako,
usaidie hawa wawili kujuana na kufahamiana
zaidi na zaidi kila siku,
ili wafuate Yesu na umoja na furaha,
Kwa jina lake aliyekufa kutukomboa,
Yesu Kristo. **Amina.**

B *Kwa kuzaa watoto*

Baba ya mbinguni,
muumba wa vitu vyote,
unatuwezesha kushiriki nawe kwa kazi ya kuumba.
Uwabariki watu hawa na zawadi ya kuzaa na kutunza watoto,
wenye watafurahisha na kusaidia wazazi kwa miaka ijayo;
na wenye watapenda na kutumikia Mwana wako Yesu Kristo.
Amina.

C *Kwa nyumba ya kikristo*

Bwana Yesu, uliyekomea kwa nyumba ya Maria na Yosefu,
ubariki nyumba ya waliofunga ndoa leo,
iwe nyumba takatifu,
makao ya salama na furaha, kweli na mapendo.
Iwe pahali pa kupumzika kwa wenye kuchoka;
pahali pa starehe kwa wenye kuteswa;
pahali pa mapendo kwa wenye kuchukiwa;
na pahali pa kutangaza Habari Njema ya uzima wa milele.
Amina.

D *Kwa watoto na wazazi*

Baba ya wote,
ni kwa mapenzi yako wazazi na watoto wanatumikiana katika mapendo;
usaidie wazazi, waweze kulea na kufundisha watoto wao,
pasipo kuwachokoza,
na pasipo kuzuiza uhuru wao katika Kristo;
usaidie watoto kutii wazazi na unyenyekevu,
na waliokomea kuheshimu wazee wao;
wote wapate heri, na kuishi siku nyingi duniani;
wakikumbuka wewe,
Muzazi wa wazazi wote,
mwenye utukufu daima,
pamoja na Mwana na Roho Mutakatifu. **Amina.**

E *Juu ya mali ya ndoa*

Tunakushukuru siku zote, Mungu wa milele,
kwa sababu mapendo yako hayana mwisho,
na hatuwezi kuhesabu zawadi zako kwetu.
Na leo tunakushukuru kwani mume huyu ametoa mali
kama alama ya heshima na mapendo
kwa jamaa ya muke wake.
Umusaide kuongeza furaha yao,
na kujenga umoja kati ya jamaa hizi mbili.
Kwa jina la Mwokozi wetu Yesu Kristo. **Amina.**

20 *SALA YA BWANA. Muhudumu aseme:*

Tuombe, kama Mwokozi wetu alivyotuagiza na namna alivyotufundisha, tusubutu kusema:

Wote **Baba yetu, uliye mbinguni,**
jina lako litukuzwe,
ufalme wako uje,
mapenzi yako yatimizwe,
duniani kama mbinguni.
Utupe leo chakula chetu cha kila siku;
utusamehe makosa yetu,
kama tunavyowasamehe waliotukosea.
Usitulete katika majaribu,
lakini utuokoe katika uovu.
Kwani kwako ufalme,
uwezo na utukufu,
milele na milele, Amina.

21 *Kutia sahihi kwa Cheti cha Ndoa. Wimbo au zaburi inaweza kuimbwa.*

22 *Wimbo wa sadaka*

23* *Ikiwa ndoa inafungwa pamoja na Ushirika, inafaa sasa kufuata taratibu ya Ushirika, kwanza kukiri zambi, N°7-8, ukurasa 48, halafu kusema Salama N°21 ukurasa 56, na kuendelea hata sala baada ya ushirika N°29; na kurudi hapa chini kwa N°24.*

24* *Matangazo*

25* *Watu wanaweza kutoa zawadi za arusi.*

26* *Wazazi wa mume na muke wanaweza kuleta mashauri yao.*

27 *Kasisi aseme kwa bwana na bibi arusi:*
J na J, muende sasa katika mapendo na salama,
kufuata na kutumikia Yesu.
Mume na muke wajibu pamoja:
Roho yake awe nasi, hata milele!

28 *Kasisi aombe baraka kwa watu wote:*
Mungu Utatu Mutakatifu,
awape nguvu katika imani na mapendo,
awalinde kwa kila upande,
na awaongoze katika kweli na salama;
na baraka ya Mungu Mwenyezi,
Baba na Mwana na Roho Mutakatifu,
iwe kwenu, na ikae nanyi milele.
Amina.

29* *Wimbo wa kumaliza ibada.*